



**New Vision**  
SPECIALIST EYE CLINIC

## **MUHTASARI WA MATOKEO JUMLA YA WAGONJWA WA PRESHA YA MACHO WALIOPATA MATIBABU KWA MARA YA KWANZA KATIKA KLINIK YA NVSEC - MWAKA 2017**

1. JUMLA YA WAGONJWA WENYE PRESHA YA MACHO WALIOPATA MATIBABU KWA MARA YA KWANZA HAPA NVSEC WALIKUWA; 100 WANAUME; 58 (58%) WANAWAKE; 42 (42%)
2. MIONGONI MWA WALIOFIKA WAKIWA WANAJITAMBUA KUWA NA PRESHA YA MACHO; 74 (74%)
3. MUDA WA KUFHAMIKWA KUWA NA PRESHA YA MACHO; MWEZI 1 MPAKA MIKA 21
4. MIONGONI MWA WALIOFIKA WAKIWA WAPO KWENYE MATIBABU YA PRESHA YA MACHO; 70 (70%)
5. HALI YA UONI WALIPOFIKA: 77 (77%) UONI MZURI, 9 (9%) ULEMAVU WA KUTOKUONA KATIKA MACHO YOTE MAWILI, NA 45 (45%) ULEMAVU WA KUTOKUONA KATIKA JICHO MOJA
6. UKUBWA WA UGONJWA KWA KIPIMO CHA MADHARA KATIKA MSHIPA WA FAHAMU YA UONI; 74 (74%) WALIKUWA NA MADHARA MAKUBWA.
7. MATIBABU WALIYOPATIWA; MATIBABU KWA KUTUMIA DAWA 69 (69%), OPERESHENI 31 (31%)
8. IDADI YA WALIOJITOKEZA KUPATA OPERESHENI 17/31 (55%)
9. WASTANI WA KIWANGO CHA PRESHA YA MACHO WALIYOKUWA NAYO WAKATI WANAPATIWA MATIBABU KWA MARA YA KWANZA HAPA KLINIK (NVSEC); **25mmHg**, NA KWA WAGONJWA 66 WALIOENDELEA KUWA NA MAHUDHURIO YA HAPA KLINIK BAADA YA MWAKA MMOJA KILIKUWA; **16mmHg**.
10. IDADI YA WAGONJWA WALIOENDELEA KUPATA HUDUMA KATIKA KLINIK YETU; 66 (66%), NA WAGONJWA; 34 (34%) HAWAKURUDI

### **HITIMISHO**

Kwa ujumla kundi la wagonjwa hawa lilikuja klinik likiwa na hali nzuri zaidi katika vigezo vya; kujifahamu kuwa na ugonjwa wa presha ya macho, unafuu katika madhara ya ugonjwa na ufanisi wa tiba waliyokwishapatiwa dhidi ya ugonjwa wa presha ya macho wakilinganishwa na wagonjwa kama hao waliopata matibabu katika nyingi ya Klinik zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara kwenye miaka ya mwanzoni mwa 2000.

Hii ina maanisha kuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo matibabu haya ya presha ya macho yamekuwa yakipatikana mfululizo na kwa muda mrefu kuna matokeo chanya ya kuzuia madhara ya ugonjwa huu na kuwalinda wagonjwa dhidi ya ulemavu wa kutokuona wa kudumu. **HIVYO NI MUHIMU TIBA IWE MUAFKA NA ENDELEVU, NA WAGONJWA WAFHAMU UMUHIMU WA KUFUATILIA MATIBABU YAO.**